



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Kumb.Na.BA.1/25/01A/38

11 Juni, 2026

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Tume ya Utumishi Serikalini inatangaza nafasi ya kazi katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba kama ifuatavyo:-

1. Afisa Mipango Daraja la II – (ZPSF 02) Nafasi 1 – Pemba

Sifa za Muombaji:

- Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka arobaini na sita 46.
- Awe amehitimu Shahada ya kwanza ya Mipango au Uchumi kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Jinsi ya Kuomba:

- Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya Kielektroniki kwenye mfumo wa Maombi ya Ajira (ZanAjira) kupitia anuani ifuatayo: <https://portal.zanajira.go.tz> kuanzia tarehe **11 Juni, 2026** hadi tarehe **25 Juni, 2026**.
- Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Tume ya Utumishi Serikalini www.zanajira.go.tz.
- Barua za maombi zitumwe kwa anuani ifuatayo kupitia mfumo wa ZanAjira (kwa njia ya kielektroniki pekee):-

KATIBU,

TUME YA UTUMISHI SERIKALINI,

S.L.P 1587,

ZANZIBAR

- Muombaji anatakiwa kuainisha nafasi ya kazi anayoiomba.

- Muombaji atakaewasilisha “Progressive Report” au “Statement of Results” pekee maombi yake hayatazingatiwa.
- Kwa msaada wa kitaalamu wasiliana na Tume ya Utumishi Serikalini kupitia simu Nam. 0773101012.

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:
KATIBU,
TUME YA UTUMISHI SERIKALINI.
ZANZIBAR**